# UMOJA - JARIDA

UNITED NATIONS TANZANIA

Toleo la 84
May - Juni 2019

## SIKU YA KIMATAIFA YA ELIMU KUHUSU UALBINO




Wataalamu wa afya wakitoa huduma ya bure ya macho kwa watu wanaoishi na ualbino wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Elimu kuhusu Ualbino. Maadhimisho hayo yalifanyika mkoani Morogoro. **Picha | Lisa Brown/UN Tanzania**

Siku ya Kimataifa ya Elimu kuhusu Ualbino inaadhimishwa kila tarehe 13 Juni kwa lengo la kukuza uelewa wa watu kuhusu ualbino na kuzuia mashambulizi na ubaguzi wanaofanyiwa watu wanaoishi na ualbino. Ujumbe mkuu katika maadhimisho ya kimataifa ya mwaka huu ni *'Kuendelea Kuwa Imara'* wakati ambapo ujumbe katika ngazi ya kitaifa ulikuwa:

*"Afya Bora na Ustawi kwa Wote: Tanzania bila Saratani ya Ngozi kwa Watu wenye Ualbino Inawezekana".*

***Inaendelea Ukurasa wa pili (2)***

## VIDOKEZO

- Juhudi za kuimarisha afya ya mama na mtoto Mkoani Simiyu
- UNDP, ILO zaendesha mafunzo ya uwezeshaji vijana na wanawake kiuchumi Kigoma
- Makubaliano yafikiwa kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari Tanzania wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani

## Kauli ya Serikali

***"Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Timu ya UN na Balozi za Ireland na Norway kwa kuendelea kusaidia katika juhudi za kuleta maendeleo kupitia Programu ya Pamoja ya Kigoma na nyinginezo katika mko wangu. Watu wa Kigoma wanashukuru sana kwa ukarimu huu,"***

**Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Mh. Emmanuel Maganga, akizungumza wakati wa Mkutano wa Kamati ya Uongozi ya Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP) mjini Kigoma, Juni 26, 2019.**

*Kutoka ukurasa wa kwanza (1)*

Nchini Tanzania, Siku ya Kimataifa ya Elimu kuhusu Ualbino imekuwa ikiadhimishwa tangu mwaka 2006 katika kipindi ambacho Chama cha Wenye Ualbino Tanzania (TASA) na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali (AZAKI) yalipoanza kampeni kutetea haki za watu wenye ualbino. Maadhimisho ya mwaka huu yalifanyika mkoani Morogoro na ujumbe wa kitaifa ulilenga kuangazia kwamba watu wenye ualbino wanaweza kuishi maisha yao pasipo kupata saratani ya ngozi ikiwa watachukua hatua stahiki. Hii inaendana na Lengo la Tatu la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs): *Afya Bora na Ustawi wa Jamii.*

Akizungumza wakati wa maadhimisho hayo kwa niaba ya Makamu wa Rais, Mh. Samia Suluhu Hassan, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dkt. Steven Kebwe, alisema kwamba: “Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutoa huduma za jamii kwa watu wenye ualbino, na eneo moja ambalo Serikali inaliweka mkazo sana ni kuondoa hatari ya saratani ya ngozi kwa watu wenye ualbino.”

Kwa upande wake, Mshauri wa Uratibu wa UN Tanzania, Bw. Helge Flard, alisisitiza akisema kwamba: “Tunapaswa kusimama imara kwa ajili ya kutetea haki za watu wanaoishi na ualbino. Kila mmoja wetu anaweza kusimama imara. Sisi sote tunaweza kuchukua hatua katika maisha yetu ya kila siku na kutetea haki zinazotulinda sisi sote.”

Ni wajibu wetu kushikamana na watu wenye ualbino na kuwalinda dhidi ya ubaguzi na vitisho. Ni muhimu kulaani imani za kishirikina na za upotoshaji na wakati huohuo taasisi za sheria ziimarishe mifumo yao ili kuhakikisha kwamba watu wenye ualbino wanakuwa salama. Utetezi zaidi unahitajika ili kuwajengea uwezo watu wenye ualbino ili watambuliwe na jamii nzima kama watu wenye umuhimu katika jamii hiyo.



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dkt. Steven Kebwe (kulia); Naibu Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu (Anayeshughulika na Wenye Ulemavu), Mh. Stella Ikupa; na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bi. Regina Chonjo (kushoto) wakitembelea banda la Chama cha Wenye Ualbino Tanzania ambamo kulionyeshwa kazi za kuimarisha ubora wa maisha ya watu wanaoishi na ualbino. **Picha | Lisa Brown/UN Tanzania**



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021



Watoto wakitembelea moja ya mabanda ambayo yalikuwa yakitoa bure mafuta maalumu ya wenye ulemavu kujikinga dhidi ya jua ili kuhimiza ujumbe mkuu wa mwaka huu hapa nchini katika Siku ya maadhimisho ya Elimu kuhusu Ualbino, uliosema: 'Afya Bora na Ustawi kwa Wote: Tanzania bila Saratani ya Ngozi kwa Watu wenye Ualbino Inawezekana'. **Picha | Lisa Brown UN Tanzania**

## JUHUDI ZA KUIMARISHA AFYA YA MAMA NA MTOTO MKOANI SIMIYU

Kituo cha Afya cha Nguliati ni miongoni mwa vituo 38 vya afya ambavyo vimeimarishwa na kupewa vifaa tiba katika Mkoa wa Simiyu na Mfuko wa Idadi ya Watu Duniani wa Umoja wa Mataifa (UNFPA) kwa kushirikiana na serikali na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA). Lengo la ukarabati na utoaji vifaa hivyo ni kuimarisha afya ya mama na mtoto kwa kutoa huduma kamili za dharura kwa uzazi pingamizi na matunzo ya mtoto (CeMONC). Ili kuupa nguvu uwekezaji huo katika miundombinu, UNFPA imesaidia utoaji mafunzo kwa watoa huduma katika suhula hizo zilizoimarishwa. Mafunzo hayo yamesaidia kuimarisha uwezo wao wa kutoa huduma bora za matunzo ya afya, ikwemo CeMONC. Vilevile, magari matatu ya wagonjwa yamenunuliwa kwa ajili ya wilaya za Bariadi, Itilima na Maswa, ili kuimarisha mfumo wa rufaa na kupunguza ucheleweshwaji wa akina mama wajawazito kupata huduma sahihi.

Ngaliati, ambayo ilianzishwa kama zahanati mwaka 1988, ilipandishwa hadhi kuwa kituo cha afya mwaka 2014, ambapo kina wataalamu 10 wa afya wenye mafunzo na majengo mawili, jengo moja ni kwa ajili ya wagonjwa wa nje na lingine ni kwa ajili ya uzazi na afya ya watoto.

*Inaendelea Ukurasa wa Nne (4)*

*Kutoka ukurasa wa tatu (3)*

Kabla ya kupandishwa hadhi, wanawake waliokuwa wakihitaji huduma za dharura wakati wa ujauzito, ikiwemo kuzaa kwa upasuaji, walipewa rufaa kwenda Hospitali ya Mkoa, ambayo iko umbali wa takribani kilometa 40 kule Bariadi.

Mganga Mkuu wa Kituo cha Afya cha Nguliati, Dkt. Lameck Rsuhinye, ameshuhudia mabadiliko katika kituo hicho kutoka kuwa zahanati hadi kuwa kituo chenye chumba cha upasuaji kinachofanya kazi na wadi ya uzazi. "Changamoto katika kutoa matunzo ya huduma za dharura na magonjwa yote hapa kituoni kabla ya mabadiliko haya yaliwakatisha tamaa wanawake kuja kujifungulia hapa au hata kuja kwa huduma za afya za kabla ya kujifungua," alisema Dkt. Rsuhinye.

Kukabiliana na vifo na magonjwa yanayozuilika ya akina mama na watoto bado ni changamoto kubwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwezi Mei, 2019, kampeni ya "Jiongeze Tuwavushe Salama" iliyozinduliwa kitaifa mwaka 2018 ilifika Mkoani Simiyu, jambo linalodhihirisha mwendelezo wa ushirikiano kati ya Serikali, UNFPA na washirika wake katika kutoa kipaumbele kwa upatikanaji kwa wote wa huduma za afya ya uzazi, afya ya akina mama, watoto wachanga na watoto wengine.

> *"Changamoto katika kutoa matunzo ya huduma za dharura na magonjwa yote hapa kituoni kabla ya mabadiliko haya yaliwakatisha tamaa wanawake kuja kujifungulia hapa au hata kuja kwa huduma za afya za kabla ya kujifungua,"*
>
> **Dr. Lameck Rsuhinye, Mganga Mkuu wa Kituo cha Afya cha Nguliati**



Wataalamu wa afya waliopata mafunzo kutoka UNFPA mkoani Simiyu walipambana kwa zaidi ya saa nzima ili kuokoa uhai wa Maria na mtoto wake. **Picha | UNFPA Tanzania**



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

# WAKATI WA KUTIMIZA DIRA YA ICDP KWA WASIONUFAIKA NA AHADI YA CAIRO NI HUU




Kiongozi wa Vijana Waliobalehe wa UNFPA kwa upande wa Zanzibar, Amina Kheri, na Mwenyekiti wa AfriYAN, Dianarose Leonce Lyimo, wakihamasisha juhudi za UNFPA ili kuongeza kasi ya ahadi ya ICPD. **Picha | UNFPA Tanzania/Jacqueline Mahon.**

> *"Huu ndiyo wakati wa kupata haki, kuishi tunavyopenda, na utu kwa kila mmoja pasipo kumwacha yeyote ynuma,"*
>
> **Jaqueline Mahon, Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA)**

"Huu ndiyo wakati wa kupata haki, kuishi tunavyopenda, na utu kwa kila mmoja pasipo kumwacha yeyote ynuma," alisema Jaqueline Mahon, Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) nchini Tanzania, wakati akitoa wito wa vuguvugu la kutimiza ahadi ya Cairo ili kuihuisha.

Alikuwa akizungumza mwishoni mwa mwezi Juni katika tukio maalumu la kuadhimisha kumbukumbu ya 25 ya Kongamano Kubwa la Kihistoria la Kimataifa kuhusu Idadi ya Watu na Maendeleo (ICDP), ambalo lilifanyika jijini Cairo, Misri mwaka 1994. UNFPA Tanzania ilitoa wito kwa serikali, washirika wa maendeleo na vijana kuweka ahadi zinazotekelezeka katika kufikia dira ya ICDP kwa wale ambao bado hawajanufaika na ahadi ya Cairo.

Mkutano huo uliowaleta pamoja maofisa wa serikali, washirika wa maendeleo, mashirika ya Umoja wa Mataifa, asasi za kiraia na vijana uliangazia Mpango wa UNFPA wa Nairobi,


*Inaendelea Ukurasa wa sita (6)*

*Kutoka ukurasa wa tano (5)*

Katika mkutano uliozaa ICPD jijini Cairo miaka 25 iliyopita, serikali 179 zilipewa wito wa kuhakikisha watu wote wanapata matunzo kamili ya afya ya uzazi, yakiwemo uzazi wa mpango wa hiyari, huduma za mimba na uzazi salama. Juhudi za vuguvugu la haki ya uzazi limechangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza idadi ya mimba zisizotarajiwa na vifo vya akina mama, na imeandaa njia ya kupatikana kwa mamilioni ya watu wenye afya na mchango bora zaidi.

Nchini Tanzania, idadi ya wanawake walioolewa wanaochagua kutumia haki yao ya kutumia njia za kisasa za kuzuia mimba zisizotarajiwa imekuwa ikiongezeka hatua kwa hatua kutoka asilimia 13 hadi asilimia 32 katika muongo uliopita. Leo, asilimia 63 ya wanawake wanajifungulia katika vituo vya afya na asilimia 64 hujifungua kwa kusaidiwa na mkunga mwenye mafunzo rasmi.

Bado kuna safari ndefu ya kufikia malengo ya vuguvugu la dunia la haki ya uzazi.
Ili kuamsha utashi wa kisiasa na upatikanaji wa fedha ili hatimaye kutekeleza Programu ya ICDP kwa Vitendo, serikali za Kenya na Denmark, pamoja na UNFPA zitaandaa mkutano mkubwa jijini Nairobi kati ya tarehe 12 na 14, Novemba. Mkutano huo utaweka mkazo katika uchukuaji wa hatua thabiti ili kufikia malengo ya 'ziro tatu': kumaliza mahitaji ambayo hayajatekelezwa bado kwa ajili ya uzazi wa mpango; kumaliza vifo vya akina mama vinavyozuilika; kumaliza vitendo vya ukatili kwa msingi wa jinsia na tabia zisizofaa dhidi ya wanawake na wasichana.




Mpango Elekezi wa UNFPA wa Nairobi ukiangazia matukio nchini Tanzania katika kuelekea kwenye maadhimisho yatakayofanyika katika Mkutano wa Nairobi nchini Kenya mwezi Novemba. **Picha | UNFPA Tanzania**



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

# PROGRAMU YA UANAGENZI YA ILO YATOA MAFUNZO KWA WASIMAMIZI 110 WA HOTELI HUKO ARUSHA NA ZANZIBAR




Wasimamizi wa hoteli na wakufunzi kutoka katika hoteli na nyumba za starehe 13 wakiwa katika warsha ya TOT jijini Arusha. **Picha | ILO**

Programu ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) ya Kuongeza Ubora wa Ujuzi ya Uanagenzi katika Biashara ya Utalii ilizindua warsha ya Kutoa Mafunzo kwa Wakufunzi (TOT) huko Arusha na Zanzibar mwezi Juni, 2019. Warsha hiyo ilikuwa sehemu ya mpango wa ILO wa kujenga uwezo ili kuwapa wasimamizi wa hoteli na wakufunzi ujuzi wa kuwaongoza kwa ufanisi Wanagenzi wakati wa mafunzo kazini.

Zaidi ya wasimamizi 110 wa hoteli kutoka katika hoteli washirika 31 walishiriki katika programu ya mafunzo shirikishi ya siku sita iliyolenga kujenga uwezo wa washirika katika tasnia ya biashara za hoteli. Awamu ya kwanza ya mafunzo ilifanyika Arusha na ililenga wasimamizi 40, wakati ambapo katika ile ya Zanzibar walishiriki 70.

Wanagenzi walijiandikisha katika programu ya mafunzo kazini na kutumia asilimia 60 ya muda wao kwenye mafunzo katika hoteli washirika zilizochaguliwa. Kwa hiyo, ni muhimu kwa wakufunzi kupata msaada sahihi ili kuwezesha utoaji wa mafunzo katika muda halisi wa kazi. “Ni muhimu kwamba washirika wetu waelewe upekee wa mafunzo ya Uanagenzi. Wanagenzi si wafanyakazi wa kudumu, na wala si wanafunzi walio kwenye mafunzo kazini au wanafunzi na kwa hiyo hawawezi kuchukuliwa kuwa hivyo,” alieleza Bw. Comoro Mwenda, Ofisa wa Programu wa ILO, Uendelezaji wa Ujuzi.

Ili kuwaelekeza na kutoa mafunzo kwa washirika wa tasnia, mafunzo yalikazia, miongoni mwa mambo mengine, kutambulisha dhana ya uanagenzi, kubaini mahitaji ya mafunzo na kutayarisha na kuwezesha mafunzo ya uanagenzi. Warsha zilijumuisha ujifunzaji kwwenye mwelekeo wa ushirikishwaji, utaratibu unaowaruhusu wakufunzi na wasimamizi kubadilishana uzoefu na maarifa.

Jovita Dallaris, Mkufunzi Mwandamizi katika Chuo cha Utalii cha Arusha anasema kwa hakika mafunzo hayo yamekuja katika wakati mwafaka. “Viwango katika tasnia ya uendeshaji hoteli vimeshuka kadiri miaka inavyopita, yatupasa kufanya kazi sana ili kurudisha mapenzi na kujituma zaidi ili kuweka mkazo katika utoaji wa huduma bora kabisa. Programu kama hizi siyo tu njia ya kupata mafunzo bali pia kushirikishana maarifa na uzoefu na kubadili namna tunavyofanya kazi yetu kama wakufunzi,” alisema.

Programu ya Uanagenzi inagharimiwa na serikali ya Norway na mafunzo pia yanasaidiwa na Chama cha Wawekezaji katika Utalii Zanzibar (ZATI) na Chuo Kikuu cha Serikali cha Zanzibar (SUZA) pamoja na Chama cha Wanye Hoteli Tanzania (HAT) na Chuo cha Taifa cha Utalii cha Tanzania Bara (NCT).

# MKUTANO WA KAMATI YA UONGOZI YA KJP



Waziri wa Mambo ya Ndani Kangi Lugola akiongoza matembezi ya Siku ya Wakimbizi Duniani jijini Dar es Salaam. Wengine ni pamoja na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Meja Jenerali Jacob Kingu, Mwakilishi wa UNHCR nchini Tanzania, Bi. Chansa Kapaya na Kamishna Jenerali wa Magereza Phaustine Kasike. **Picha | UNHCR**

*Inaendelea Ukurasa wa tisa (9)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa nane (8)*



Kikundi cha Wapiga Ngoza za Asili wa kutoka Kongo wakitumbuiza kwa wimbo wa asili wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wakimbizi Duniani katika Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma. **Picha | Edgar Kiliba/UN Tanzania**

# RIPOTI MAALUMU II
# MKUTANO WA KAMATI YA UONGOZI YA KJP




Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali Mstaafu Emmanuel Maganga (kushoto) akifungua rasmi Mkutano wa Kamati ya Uongozi ya Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP). Brigedia Jenerali Maganga, ambaye ndiye mweneyekiti wa kamati hiyo, alisema kwamba tayari KJP imeanza kuzaa matunda baada ya utekelezaji wa takribani miaka miwili.
*** Picha zote na Edgar Kiliba/UN Tanzania & Msafiri Manongi/UN Tanzania**

Mwezi Juni, mamlaka ya serikali ya mkoa wa Kigoma iliwapokea wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Progamu ya Pamoja ya Kigoma (KJP). Waliwakaribisha maofisa kutoka Ubalozi wa Norway, Ubalozi wa Ireland, Umoja wa Mataifa na maofisa wengine kutoka serikalini ikiwemo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na wale wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) katika Mji wa Kigoma ambako ndiko ulikofanyika mkutano huo.

Huu ulikuwa mkutano wa kwanza wa Kamati ya Uongozi ya KJP tangu nchi ya Ireland ilipojitolea kuyapa Mashirika ya Umoja wa Mataifa jumla ya Dola za Marekani milioni 20 kwa ajili ya Afya, Lishe na VVU (Afya+), ambacho ni kipengele cha saba katika KJP ambacho kilipitishwa na kamati mwezi Januari, na pia uchukuaji wa hatua wa UN katika sekta ya afya katika maeneo mengine ya nchi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya KJP, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali (Mstaafu) Emmanuel Maganga alisema kwamba tayari KJP imeanza kuleta matunda katika kipindi chake cha utekelezaji cha miaka miwili.

***Inaendelea Ukurasa wa kumi na moja (11)***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa kumi (10)*

"Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Timu ya UN na kwa Balozi za Ireland na Norway kwa msaada ambao wanaendelea kutoa katika kusukuma maendeleo kupitia Programu ya Pamoja ya Kigoma na juhudi nyinginezo katika mkoa wangu. Watu wa Kigoma wanatoa shukurani zao za dhati kwa ukarimu huu," alisema Brigedia Jenerali Maganga.

Kwa upande wake, Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez, aliishukuru serikali na pia washirika wa maendeleo kwa kuendelea kufadhili KJP. Alitoa changamoto kwa mashrika ya Umoja wa Mataifa kuendelea kushirikiana miongoni mwao pamoja na wenzao wa serikalini ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Mpango huo unakuwa wenye mafanikio. "KJP imekuwa ikiinua viwango vya maisha ya jamii za wenyeji ambao kwa miongo mingi wamewakaribisha wakimbizi," alisema.

Baada ya kuhitimishwa kwa mkutano, wajumbe walitembelea maeneo kadhaa ambako shughuli za utekelezaji wa mpango na serikali, mashirika ya UN na washirika wengine unaendelea kama sehemu ya KJP na juhudi nyingine na pia walitembelea Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu ili kuadhimisha Siku ya Wakimbizi Duniani. Picha za ziara hii katika maeneo mbalimbali ziko katika kurasa mbili zinazofuatia.




Meneja wa Programu wa Afya ya Uzazi na Lishe wa Ubalozi wa Ireland, Bi. Kim Mwamelo (katikati), alisema kwamba KJP ni mfano bora wa ushirikiano kati ya serikali, washirika wa maendeleo na mashirika ya Umoja wa Mataifa ili kufikia lengo moja. Nchi ya Ireland imeahidi kutoa Dola za Marekani milioni 20 kwa ajili ya kipengele cha Afya+ cha Programu ya Pamoja ya Kigoma ambacho kinahusisha maeneo ya Afya, VVU na Lishe.

# KIGOMA JOINT PROGRAMME - FIELD VISITS



Mwakilishi wa UN Women (Wanawake), Bi. Hodan Addou (katikati) na Mkurugenzi Msaidizi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Emmanuel Nyingi (kulia), wakipanda mti mbele ya Dawati la Jinsia ambalo linatarajiwa kuanza kufanya kazi katika miezi michache ijayo.



Hapa, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali Mstaafu Emmanuel Maganga akikagua vibanda vipya kwa ajili ya wafanyabiashara ambavyo vimejengwa na Kituo cha Kimataifa cha Biashara (ITC). Vibanda hivi vitajengwa katika eneo lote la ndani la soko na vitakuwa na sehemu ya kuhifadhia bidhaa ili wafanyabiashara wawe na mahali salama pa kutunza mizigo yao pale wanapofunga biashara jioni.



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

# KIGOMA JOINT PROGRAMME - FIELD VISITS



Kupitia juhudi za ILO na UNDP, kikundi hiki kimeweza kuimarisha ujuzi wao katika maeneo ya utunzaji kumbukumbu, upigaji hesabu za gharama na mikakati ya utafutaji masoko, miongoni mwa mambo mengine. Pia, wamepokea takribani Dola za Marekani 7,000 kama msaada ambao wameutumia kununua vyerehani vipya, vifaa na kumudu gharama nyingine za uendeshaji miongoni mwa mambo mengine. Kwa sababu ya msaada huo uzalishaji wao na faida vimeongezeka na fedha inayopatikana inawasaidia kujipatia mahitaji ya kaya zao yanayohusiana na elimu na megineyo.



Wanawake hawa kutoka Wilaya ya Kasulu wanafundishwa kushona kwa cherehani kupitia Programu ya Kisheria ya Kuwaingiza Vijana Wailiobalehe na Kuacha Shule (IPOSA) ambayo hivi sasa inatekelezwa na UNICEF chini ya Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP). Ujumbe ulipata fursa ya kutazama moja ya kipindi chao na kisha kuonja juisi, vitafunwa vilivyotengenezwa wakati wa vipindi vya mapishi kama sehemu ya programu.

# MAKUBALIANO YAFIKIWA KUIMARISHA UHURU WA VYOMBO VYA HABARI TANZANIA WAKATI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA UHURU WA VYOMBO VYA HABARI DUNIANI




Balozi wa Uingereza, Mh. Sarah Cooke, akizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani (WPFD) ya mwaka 2019. Aliangazia umuhimu wa kuwa na vyombo vya habari vilivyo huru na wazi. **Picha | Edgar Kiliba/UN Tanzania**

*“Tumedhamiria kwamba Uingereza itakuwa mpigania nambari moja wa uhuru wa vyombo vya habari duniani. Ndiyo sababu Uingereza inaunga mkono matukio haya ya leo kwa sababu sisi tunaamini kwamba yatupasa kufanya kazi pamoja ili kukabiliana na upotoshaji wa habari na kuhamasiha ukweli,”*

**Mh. Sarah Cooke, Balozi wa Uingereza, Tanzania**

“Tumedhamiria kwamba Uingereza itakuwa mpigania nambari moja wa uhuru wa vyombo vya habari duniani. Ndiyo sababu Uingereza inaunga mkono matukio haya ya leo kwa sababu sisi tunaamini kwamba yatupasa kufanya kazi pamoja ili kukabiliana na upotoshaji wa habari na kuhamasiha ukweli,” alisema Mh. Sarah Cooke, Balozi wa Uingereza nchini, wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habri Duniani (WPFD) ya 2019.

Mwaka huu, zaidi ya wadau na washirika mia tatu kutoka katika vyuo vya juu, serikalini na vyama vya kiraia walikutanika jijini Dodoma ili kujadiliana masuala yanayohusu mada ya dunia, ambayo ni: ‘Vyombo vya Habari kwa ajili ya Demokrasia: Uandishi wa Habari na Uchaguzi katika Zama za Upotoshaji Habari’.

Kongamano hilo la kitaifa lilileta matokeo ambapo serikali iliahidi kushiriki katika majadiliano na wadau wa vyombo vya habari ili kuiamarisha ushirikiano katika kukuza uhuru wa vyombo vya habari,

***Inaendelea Ukurasa wa kumi na tano (15)***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa kumi na nne (14)*

yakiwemo masuala yanayohusu usalama wa waandishi wa habari. Ubalozi wa Uingereza nchini Tanzania uliahidi kutos Shilingi bilioni 7.8 (takribani Dola za Marekani milioni 3.4) ili kusaidia kuimarisha vyombo vya habari na nafasi kwa vyombo vya kiraia nchini Tanzania.

UNESCO pia itashirikiana na Serikali na washirika katika masuala muhimu yaliyokubaliwa ya kuimarisha majadiliano kati ya serikali, wadau wa vyombo vya habari na washirika kuhusu kuimarisha nafasi ya vyombo vya habari na asasi za kiraia; kusaidia uchukuaji hatua kwa kuzingatia data ili kukuza vyombo vya habari; na kuhamasisha usawa wenye haki katika jinsia kupitia vyombo vya habari.

Katika maadhimisho ya kitaifa, Lengo la 16 la SDG, ambalo linazibana Nchi Wanachama wa UN kuhakikisha "umma unapata taarifa na kulinda uhuru wa msingi, kwa mujibu wa sheria za kitaifa na mikataba ya kimataifa", liliangaziwa. Viashiria viwili vya lengo hili vinalenga hasa kuhakikisha maendeleo katika usalama wa waandishi wa habari na hakikisho la kisheria na kisiasa la upatikanaji wa taarifa.

Jukumu muhimu la vyombo vya habari ni kama lilivyoelezwa na Kaimu Balozi wa Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania, Bi. Imni Patterson, kuwa ni kiini cha kujenga jamii endelevu, wakati alipokuwa akitoa mada katika kipindi ambacho kilifunguliwa na Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Hassan Abbasi.



Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Hassan Abbasi (kushoto) akitembelea maonyesho ya Umoja wa Mataifa Tanzania wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani yaliyofanyika Jijini Dodoma, ambapo alipokelewa na Ofisa Habari wa Kituo cha Habari cah UN (UNIC), Bi. Stella Vuzo (kulia).

# UNDP, ILO ZAENDESHA MAFUNZO YA UWEZESHAJI VIJANA NA WANAWAKE KIUCHUMI KIGOMA



Wawakilishi wa biashara 12 ambazo zilishiriki katika mafunzo ya siku nane ya uwezeshaji kiuchumi vijana na wanawake katika Wilaya ya Kasulu. **Picha | ILO**

Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kushirikiana na Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP) liliendesha programu ya mafunzo kwa wajasirimali ya siku nane kwa vikundi 12 vya kibiashara huko Kigoma, mwezi Juni. Mafunzo hayo yalioandaliwa kupitia kipengele cha Uwezeshaji Vijana na Wanawake Kiuchumi, ambacho ni sehemu ya Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP), yalilenga wanufaika 24 kutoka katika wilaya nne za Mkoa wa Kigoma. Warsha hiyo ni sehemu ya juhudi ya kujenga uwezo ya Programu hiyo ambayo inalenga kutoa masaada endelevu na uelekezi kutoka kwa mwenye uzoefu kwa wanawake na vjana 289 (miongoni mwao asilimia 85 wakiwa ni wanawake), ambao walipata msaada wa fedha na pia usio wa kifedha.

Baada ya miezi sita, vikundi 12, kupitia msaada chini ya program hiyo, vilianzisha biashara mbalimbali: kama vile samaki, kuku, ufugaji nguruwe, uchakataji wa mazao ya kilimo, ubunifu wa mitindo, ushonaji na utengenezaji divai. Vikundi hivyo sasa vinapata fursa na kukabiliana na changamoto mbalimbali katika safari yao ya kujenga uwezo endelevu ili zikue na kuwa biashara ndogondogo. ILO na UNDP zinashirikiana kuvisaidia vikundi kuimarisha na kukuza biashara zao kupitia zana maalumu za ILO za Kuanzisha a Kuimarisha Biashara Yako (SIYB, yaani *Start and Improve your Business).*

"Biashara ndogondogo hivi sasa zinapitia kipindi cha mpito ambapo ujuzi wa usimamizi wa biashara ndivyo vinavyoamua kuhusu ukuaji wa biashara hizo na uendelevu wake," anasema Bi. Cressida Mwamboma, Ofisa wa Programu, Taifa.

Miongoni mwa mambo mengine, mafunzo yaliweka mkazo katika kupunguza ukosefu wa maarifa katika usimamizi wa biashara, huku mkazo mkubwa ukiwa katika kuwaelewa wateja, kuimarisha ujuzi wa watafuta masoko na kutunza kumbukumbu za biashara vizuri na akiba ya bidhaa. Wanachama wa kikundi cha kibiashara cha Vijana Tuinuane kutoka Wilaya ya Kibondo si wageni katika ulimwengu wa biashara ya kilimo lakini kule kushiriki kwao katika mafunzo kutoka katika programu ya YWEE kumewapa fursa ya kuendesha biashara zao kwa umahiri zaidi wa kibiashara. Kwa mujibu wa mwenyekiti wao, David Dauson, mafunzo ya SIYB yamewasaidia kuwa wafanyabiashara makini zaidi.

"Ninafikiri sisi kama wakulima tunasahau kuitazama kazi kwa jicho la kibiashara. Kabla ya mafunzo, sisi hatukujua kuhusu gharama za moja kwa moja za vitu na gharama zisizo za moja kwa moja, hivi sasa tunajua jinsi ya kusimamia gharma ili kuongeza faida yetu," alisema.

***Inaendelea Ukurasa wa kumi na saba (17)***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa kumi na sita (16)*

Coletha Chutse, ambaye ni kiongozi wa kikundi cha Wanawake cha Wafuga Nguruwe cha Tushirikiane anaona kwamba maarifa waliyopata ni yenye thamani kubwa sana.

“Tunawashukuru sana UNDP na ILO kwa kuzipatia biashara zetu fedha, na mafunzo tuliyoshiriki wiki hii yatatujengea uwezo kama wanawake wafanya biashara. Hivi sasa tunajenga na ujuzi tuliopata kuhusu gharama za utengenezaji bidhaa na utoaji huduma utatusaidia sana. Sisi kama wanaweke mara nyingi tunalipishwa gharama kubwa sana katika ujenzi kwa sababu wauzaji wa vifaa wanafikiri kwamba sisi ni wajinga katika masuala hayo,” alisema Coletha.

## SIKU YA USALAMA WA CHAKULA DUNIANI 2019: USALAMA WA CHAKULA UNATUHUSU SOTE



Akina mama na baba lishe wana mchango mkubwa sana katika usalama wa chakula katika jamii. Ikiwa vyakula wanavyouza havilindiwia ipasavyo, basi walaji wanaweza kuathirika vibaya sana. **Picha | ©FAO Tanzania**

Maadhimisho ya kwanza kabisa ya Siku ya Usalama wa Chakula Duniani (WFSD) yalifanyika Juni 7 na kuadhimishwa ili kutoa elimu na kushawishi uchukuliwaji wa hatua ili kuzuia, kung’amua na kumudu hatari zinazotokana na vyakula, kuchangia katika usalama wa chakula, afya ya watu, ukuaji wa kiuchumi, kilimo, upatikanaji wa masoko, utalii na maendeleo endelevu. Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FA) na Shirika la Afya Duniani (WHO), ambayo ni mashirika yanayoongoza katika kuweka viwango vya usalama wa chakula duniani ili kulinda afya za watumiaji na kuhakikisha kunakuwa a biashara yenye haki ya chakula, yaliongoza maadhimisho hayo katika siku hiyo kote duniani.

Suala la kumaliza kabisa njaa linahusu kila mtu kupata chakula salama, chenye lishe bora na cha kutosha, kwani hatuwezi kuwa na usalama wa chakula pasipo chakula hicho kuwa salama. Pale chakula kinapokuwa si salama, watoto hawawezi kusoma, watu wazima hawezi kufanya kazi. Maendeleo ya watu hayawezekani. Kupata chakula cha kutosha kilicho salama na bora ni jambo muhimu ili kuendeleza uhai na kuleta afya njema kwa kila mmoja.

Usalama wa mlo ni suala lenye athari ya moja kwa moja katika afya ya watu na ulaji wa viritubisho. Ni suala lenye umuhimu mkubwa katika kuhakikisha kwamba chakula kinabaki salama katika kila hatua ya mnyororo wa chakula kuanzia uzalishaji hadi uvunaji, uchakataji, hifadhi, usambazaji hadi kupika na kula.

Pale nchi zinapoimarisha uwezo wao wa kisheria,

*Inaendelea Ukurasa wa kumi na nane (18)*

*Kutoka ukurasa wa kumi na sita (16)*

kisayansi na kiteknolojia ili kuhakikisha milo inakuwa salama na ina ubora unaotakiwa katika mnyororo mzima wa chakula, basi zinakuwa zikielekeakatika mienendo iliyo endelevu zaidi ya uzalishaji na utumiaji chakula.

Leo, Tume ya Codex Alimentarius ya FAO na WHO ina wajibu mkubwa katika kuweka viwango vya kimataifa vya vyakula ili kuwalinda watumiaji na kuhakikisha kwamba haki inazingatiwa katika biashara nzima ya chakula. FAO na WHO pia zinatimiza wajibu muhimu katika kujenga uwezo wa ndani wa nchi ili kutekeleza mifumo ya milo salama.

Kila mmoja ana haki ya kupta chakula salama, chenye virutubisho na cha kutosha. WFSD inapaswa kuwa fursa ya kuimarisha juhudi zetu ili kuhakikisha kwamba chakula tunachokula ni salama tangu uzalishaji hadi muda wa kukitumia. Kila anayehusika katika mnyororo wa chakula ana wajibu wa kuhakikisha milo inakuwa salama. Huu ndio wakati wa kutenda!



## MATUKIO YAJAYO YA SIKU ZA KIMATAIFA

**Julai 30**
Siku ya Dunia ya Kupiga Vita Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu

**Agosti 9**
Siku ya Kimataifa ya Wenyeji wa Dunia

**Agosti 12**
Siku ya Kimataifa yaVijana

**Agosti 19**
Siku ya Kimataifa ya Ubinadamu

**Septemba 8**
Siku ya Kimataifa ya Kusoma na Kuandika

**Septemba 15**
Siku ya Kimataifa ya Demokrasia

## UMOJA WA MATAIFA MADHUBUTI KWA DUNIA BORA ZAIDI

UNITED NATIONS TANZANIA

**UN Resident Coordinator’s Office**

+255 22 219 5021

info.untz@one.un.org

www.tz.one.un.org



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021